

SOMA MPYA

OFISI YA RAISI  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHURI YA WILAYA YA IRINGA



**TANGAZO**

UKODISHAJI WA GHALA (KARAKANA) LA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA  
LILILOPO IPOGORO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

TAREHE: 18/06/2021


Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa anawatangazia Wafanyabiashara wote, Vikundi vilivyosajiliwa, Makampuni na Watu binafsi wenye uwezo na sifa za kukodi ghala (Karakana) la Halmashauri ya Wilaya Iringa lililopo Ipogoro kama ilivyo elekezwa kwenye jedwali hapa chini kwa kipindi cha mwaka fedha 2021/2022 kwa kuleta maombi yao

NAMBA YA ZABUNI	ENEO ILIPO	MAELEZO
LGA/026/2021/2022/S/05	Ipogoro	Ukodishaji wa Ghala(Karakana) ya Halmashauri ya Wilaya Iringa

**MASHARTI YA WAOMBAJI:**

1. Kila mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania.
2. Mwombaji aambatishe usajili wa TIN (au VAT)
3. Mwombaji anatakiwa awe na Leseni husika.
4. Mwombaji aambatishe uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax Clearance Certificate) ya mwaka 2020/2021
5. Uthibitisho wa uwezo wa Mwombaji kifedha kwa kuonyesha Taarifa ya Fedha ya Benki (Bank Statement) ya miezi mitatu ya hivi karibuni iliyo idhinishwa na kuthibitishwa na Meneja wa Benki ya tawi husika.
6. Mwombaji aambatishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atakaye husika na zabuni hii.

7. Taarifa ya madeni yake yote (kama yapo) anayo daiwa na watu binafsi, Benki na Halmashauri hii au nyingine katika Tanzania
8. Mwombaji anatakiwa kutokuwa na mgogoro wowote na Halmashauri.
9. Mwombaji atakayepata kazi atatakiwa awasilishe alipe/ (dhamana) fedha taslimu zinazolingana na mawasilisho ya miezi mitatu (3). Fedha hizi atarudishiwa baada ya mkataba kuisha endapo atakuwa hadaiwi.
10. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Shilingi elfu ishirini (TZS. 20,000.00) kwa kila ombi la Zabuni na kupewa stakabadhi pamoja na kabrasha la Zabuni ambalo utatakiwa kulijaza na kulirudisha kabla ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ada ya maombi hairudishwi.
11. Maombi yafungwe katika bahasha kwa lakiri (Seal) katika bahasha mbili(2) moja halisi na moja nakala na kuonesha namba za zabuni, na kuwasilisha katika, **"OFISI YA ZAMANI YA KITENGO CHA UNUNUZI ILIYO KATIKA UKUMBI WA SIASA NI KILIMO , S.L.P. 108, IRINGA"**
12. Maombi yaandikwe kwa, **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA S.L.P. 108, IRINGA.**
13. Maombi ambayo hayatazingatia masharti ya kazi iliyotajwa hapo juu hayatafikiriwa.
14. Waombaji wote wanakaribishwa kufika wenyewe au kutuma wawakilishi wenu siku ya ufunguzi. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Katibu wa Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Wilaya Iringa.
15. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/06/2021 saa nne kamili asubuhi (4.00) na zabuni zitafunguliwa baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Iringa.

  
.....  
Bashir Paul Muhoja  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
HALMASHAURI YA WILAYA  
IRINGA**